WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Jamhuri, wakiwasilisha mada kuhusu Mashine za Risiti za Kielektroniki (EFD), wakati wa mashindano ya vilabu vya kodi yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dar es Salaam, jana. (Picha na Jumanne Gude)

UHURU UK 9.

# Serikali yatoa chanjo 2,700 za kichaa cha mbwa, paka

**Na MASHAKA MHANDO,** *Muheza*

SERIKALI imetoa chanjo 2,700 za ugonjwa wa kichaa cha mbwa na paka katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, kudhibiti ugonjwa huo ambao ni hatari kwa afya ya binadamu na wanyama.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa chanjo hiyo iliyofanyika katika Kijiji cha Mkanyageni, kilichopo Kata ya Ngomeni, juzi Mkuu wa Divisheni ya Kilimo na Mifugo, Edward Mgaya, alisema kazi hiyo ni endelevu hadi pale chanjo zitakapokwisha.

Mgaya alitoa wito kwa wananchi kuwapeleka wanyama hao vituo vilivyotengwa vilivyopo katika maeneo wanayoishi lengo likiwa ni kukabili ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

"Ugonjwa wa kichaa cha mbwa hauna tiba ila unazuilika kwa njia ya chanjo. Ugonjwa huu huwapata wanyama na binadamu kwa kung'atwa na mnyama mwenye virusi vinavyojulikana kama 'Rhabdoviridae', " alisema.

Alisema kuwepo kwa mbwa wazururaji mitaani, ufugaji wa mbwa bila kuzingatia chanjo dhidi ya ugonjwa huo na kuchokoza au kucheza na mbwa au paka ambao hawajachanjwa kuna uwezekano wa kutokea kwa ugonjwa huo.

Mgaya alizitaja dalili za mbwa mwenye ugonjwa huo ni kuhangaika na kukimbia ovyo ovyo masafa marefu huku akitokwa na mate mengi mfululizo.

Pia, kushambulia na kung'ata kitu chochote anachokutana nacho kama vile vijiti, vyuma, watu na wanyama wengine na kushindwa kula, kudhoofu, kupooza na kufa.

Ofisa Mifugo Mkuu Zakaria Swai, aliwataka wananchi kuwapeleka mbwa kupatiwa chanjo katika vituo vya afya, kuwaepusha kupata maradhi ya kichaa cha mbwa.

Alisema hadi hivi sasa chanjo 55 za kichaa cha mbwa na paka zimetolewa wilayani humo.

**Idadi**

**CHANJO**

Alisema hadi hivi sasa chanjo 55 za kichaa cha mbwa na paka zimetolewa wilayani humo.

kwa kuvitembelea na

mazao yao.

NI PASHE UK 10

# 'Usipopeleka mifugo kupata chanjo faini 300,000'

**Na Halima Ikunji,** UYUI

MKUU wa Wilaya ya Uyui mkoani Tabora, Zachalia Mwansasu amewaonya wafugaji ambao wamegoma kupeleka mifugo kwa ajili ya kupata chanjo ya mapele ya ngozi katika Kijiji cha Ibelamilundi, kwamba watakaoshindwa kutekeleza hatua hiyo watatozwa faini ya Sh.300,000.

Aliyasema hayo kwenye uzinduzi wa chanjo za mifugo ya mapele ya ngozi uliofanyika jana wilayani hapa na kusema kuwa hatamuonea haya mtu yeyote kwa kushindwa kutekeleza agizo hilo kwani atakuwa amekiuka sheria ya nchi.

Mwansasu alisema kwamba majosho 13 yamekarabatiwa na mengine manne yamejengwa na tayari wameyazindua katika maeneo ya Shitage, Upuge, Muhulidede na Mishwaki.

"Katika mwaka wa fedha 2023 serikali imetupatia fedha za kujenga majosho 13 kukarabati ya zamani na kwa mwaka huu kuna bajeti ya majosho 18, kadhalika zimetolewa fedha za ruzuku kwa ajili ya dawa za mifugo," alisema.

Meneja wa ghala wa maabara ya Vetinali Kanda ya Magharibi Tabora, Nae Dk. Kwari Bura, alisema kuwa wamezindua chanjo ya mifugo ya vipele ngozi na mpango huo ni kufuatia mpango wa kuchanja ugonjwa mmoja kila mwaka kati ya magonjwa 13.

Alisema kwamba kwa Wilaya ya Uyui walichanja mifugo kwa miaka mitatu mfululizo, huku kila ngombe mmoja akitakiwa kupata chanjo za magonjwa saba.



a jana,

nizani ya madini